# TANZANIA BILA UKATILI

SIKU 16 ZA KUPINGA UKATILI WA KIJINSIA

16 DAYS

WiLDAF

# Asante kwa kuungana nasi katika kuadhimisha kampeni ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia.

Kuanzia tarehe 25 Novemba, siku ya kwanza ya kampeni ya Kimataifa ya kupinga ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto; na kilele chake tarehe 10 Desemba,ambayo ni Siku ya Kimataifa ya Haki za Binadamu, Tanzania itaungana na wanaharakati wengine, duniani kote kuadhimisha siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia. Kampeni ya Siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia ni wakati wa kutafakari juu ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto na kuchukua hatua ili kukomesha vitendo hivo.




## Kuna njia nyingi za kushiriki katika kampeni hii:

1. Unga mkono harakati za siku 16 za kupinga Ukatili wa Kijinsia.

- Onesha ishara ya Amani! vaa fulana au shati lenye ya rangi ya chungwa (Orange).

- Shawishi familia, marafiki, majirani kushiriki katika kampeni.

- Ungana na wafanyakazi wenzio katika mijadala mbalimbali kama wakati wa chai ya asubuhi au chakula na kujadili kuhusu ukatili wa kijinsia mahala pa kazi na hata kutumia njia ya majadiliano katika mitandao ya kijamii.

- Shirikishana jumbe na picha mbalimbali za kupinga Ukatili wa Kijinsia kupitia mitandao ya kijamii ili kampeni iweze kuwafikia watu wengi zaidi

2. Ibua mijadala ya ukatili wa Kijinsia

- Anzisha dawati la jinsia shuleni kupitia club za afya na jinsia, fema au masomo(subject clubs).

- Anzisha klabu za kupinga ukatili sehemu yako ya kazi, michezoni, sehemu za ibada kama makanisani, na misikitini, ili kujadili na kupinga ukatili wa Kijinsia unaotokea majumbani.

3. Jiunge katika maadhimisho haya ya kampeni ya siku 16 za kupinga ukatili wa Kijinsia popote pale unaposikia.

- Shiriki katika kampeni ya siku 16 popote pale kwa ajili ya maendeleo ya Tanzania isiyo na Ukatili.

4. Wezesha upatikanaji wa huduma za msaada wa Kisheria

- Huduma mkoba (outreach program) za msaada wa kisheria maeneo ya vijijini ili kuwafikia wanawake wanaohitaji msaada wa kisheria, pia kuwajengea uwezo kuhusu haki na sheria mbalimbali.

- Huduma ya dawati la jinsia kwenye taasisi za elimu kama vile vyuo vikuu.

5. Chukua hatua na vunja ukimya,

- Wasaidie wahanga wa Ukatili wa Kijinsia kuepuka manyanyaso katika jamii na kupatiwa huduma za msaada wa kisheria, kisaikolojia na hata matibabu ya afya.

- Toa taarifa kwa vyombo vya dola, serikali na hata asasi za kiraia pindi unapofanyiwa au kushuhudia vitendo vya Ukatili wa Kijinsia kwa msaada zaidi wa kisheria.

## TUUNGANE KULETA MABADILIKO

• Badili rangi ya mpangilio wa tovuti na akaunti zako katika mitandao ya kijamii na kuwa rangi ya chungwa katika kipindi hiki cha siku 16 za kupinga Ukatili wa KijinsiaUngana nasi kwenye mitandao ya kijamii kupitia akaunti zetu
• FACEBOOK: www.facebook.com/WiLDAFTz
• TWITTER:  www.twitter.com/WiLDAFTz
• INSTAGRAM:  www.instagram.com/WiLDAFTz .
• WEBSITE: www.wildaftanzania.org
• Jiunge na mazungumzo. Kuwa sehemu ya mabadiliko na uangalie maudhui yaliyoshirikishwa kupitia alama za reli  (hashtags) zifuatazo:
#HerSafetyMyResponsibility
#UsalamaWakeWajibuWangu

## Wewe ni sehemu muhimu ya kuchochea na kuleta mabaliko katika harakati hizi; Tumeandaa kijarida hiki kukupa taarifa muhimu kama vile;

• Kampeni
• Jumbe muhimu
• Hali ya ukatili wa kijinsia
• Shughuli za kampeni
� Taarifa za mitandao yetu ya kijamii
� Kopi ya tovuti
� Ushiriki wa wadau wa kimataifa
� Huduma za msaada

Tuungane  kuwajibika katika kumtetea kila  mwanajamii anayefanyiwa ukatili, inaweza kuwa moja ya njia nzuri ya kuleta mabadiliko na kujenga uelewa kwenye jamii kuhusu masuala ya ukatili wa jinsia.

# KAMPENI

## MADHUMUNI

Katika kampeni ya siku 16 za kupinga Ukatili wa Kijinsia mwaka huu ni wakati wa kutafakari, kupaza sauti na kuelimisha jamii kuhusu vitendo vya ukatili wa kijinsia, madhara yake, na hatua za kuchukua kukabili vitendo hivyo. Tusikubali ukatili kuendelea sehemu za kazi, mashambani, kwenye nyumba za ibaada na hata mashuleni.
Kampeni inaleta nafasi ya kuchochea usawa wa kijinsia katika jamii, kushiriki mijadala kuhusu ukatili na kusaidia waathirika wa vitendo vya ukatili.
Kila mmoja ana wajibu wakujilinda na kulinda familia dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia katika maeneo mbalimbali kama Shuleni, nyumbani, kazini, nyumba za ibada, klabu za michezo, serikalini n.k
Mimi naweza, wewe unaweza na Sote tunaweza kuwa sehemu ya mabadiliko na kusaidia kuvunja mzunguko wa ukatili dhidi ya wanawake ,watoto na vizazi vijavyo.

## MUDA WA KAMPENI NI KUANZIA TAREHE 25 NOVEMBA MPAKA TAREHE 10 DESEMBA 2018

Kampeni hiyo imewekwa sambamba na Siku 16 za harakati dhidi ya kupinga Ukatili wa Kijinsia, zinazoratibiwa na Umoja wa Mataifa. Kampeni hii itaanza na uzinduzi wa tarehe 25 Novemba ambayo ni siku ya kimataifa ya kupinga ukatili dhidi ya Wanwake na kuhitimishwa Siku ya Kimataifa ya Haki za Binadamu Disemba 10.

Tunahitaji jamii yote kuhoji ubaguzi na, kuunga mkono usawa wa kijinsia katika mtazamo wa kijinsia.
Kila mtu ana jukumu la kuzuia ukatili unaofanyika kwenye familia,watu binafsi, shule, mahali pa kazi, nyumba za ibada, vilabu vya michezo na serikali.
Ikiwa wewe, au mtu unayejua, amefanyiwa ukatili wa kijinsia, unaweza kufika katika vyombo husika vinavotoa msaada wa Kisheria.
Unga mkono usawa wa kijinsia, heshimu na usiwe sehemu ya ukatili – vaa nguo zenye rangi ya chungwa kuonesha ishara ya Amani katika kipindi cha kampeni.




## KAULI MBIU

USALAMA WAKE: WAJIBU WANGU

Kauli mbiu, imelenga kutoa wito kwa kila mmoja kuchukua hatua, kuhoji, kupaza sauti, kupinga vitendo vya ukatili vinavyotokea kazini, mashuleni, taasisi mbalimbali, mitaani, hospitali, kwenye usafiri wa umma. Kauli mbio mwaka huu inasisitiza kwa kila mmoja

(i) KUTAFAKARI, na kuwa tayari wakati wote kupinga vitendo vya ukatili, na kutafuta njia za kuwasaidia waathirika wa ukatili.

(ii) KUCHUKUA HATUA, kuingilia kati kwa kupaza sauti dhidi ya vitendo vya ukatili.

(iii) KUHUSISHA, wadau wa maendeleo, azaki, na jamii katika kupinga vitendo ya ukatili wa kijinsia.
Rangi ya chungwa(Orange) ni rangi iliyochaguliwa na Umoja wa Mataifa. Inawakilisha mustakabali huru na hatima baadaye isiyo na ukatili wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto.
Watu wanahaswa kuvaa fulana au mashati ya rangi ya chungwa ili kuunga mkono na kumaliza ukatili katika familia.

(iv) KUSHAWISHI, Serikali na vyombo vya maamuzi kuharakisha mapitio ya maboresho ya sera na sheria kandamizi zinazochochea ukatili wa kijinsia ili kufikia malengo yaliyowekwa katika Mpango kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA)

# JUMBE

Duniani kote, ukatili wa kijinsia dhidi ya Wanawake na Watoto (VAWC) unafanyika ndani ya jamii, nyumba na familia.

- Msingi mkuu wa ukatili dhidi ya wanawake ni mamlaka tofauti ya umiliki kati ya wanaume na wanawake katika jamii, mifumo na kanuni ambazo zinasimama mfumo dume.
- Tanzania, ukatili dhidi ya wanawake inabaki kuwa changamoto kubwa na kizuizi kwa usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake.
- Ukatili dhidi ya wanawake ni jambo linalohitaji mwamko wa kisiasa ili kubadilisha mifumo dume katika ngazi ya mtu binafsi, watu walio kwenye mahusiano ya kimapenzi, familia, jamii na taasisi kwa ujumla.
- Ukatili dhidi ya wanawake huathiri wanawake katika kutambua uwezo wao na kuchangia maendeleo ya nchi.

## Hali ya ukatili wa Kijinsia.

Ukatili wa Kijinsia umeathiri familia nyingi za Kitanzania.

• Wanawake 271 kuanzia mwaka 2016 - Mei 2018 wameuawa na waume/wenzi wao kutokana na wivu wa mapenzi. (Mtanzania 3 Juni 2018)

• 40% ya wanawake wenye miaka 15-49 wamefanyiwa ukatili wa kimwili.(TDHS 2015-2016)

• Wanawake 7 kati ya 10 walioolewa ambao waliofanyiwa ukatili katika ndoa walipata majeraha. (TDHS 2015-2016)

• 1/3 ya wanawake walioolewa wamefanyiwa ukatili na waume / wenzi wao.(TDHS 2015-2016)

# UNGANA NASI KUPITIA




## Website Link

http://wildaftanzania.org/campaign/

## Facebook Page

https://www.facebook.com/WiLDAFTz

## Twitter page

https://twitter.com/WiLDAFTz

## Instagram Page

https://www.instagram.com/wildaftz/

# UNGANA NA WADAU WA KIMATAIFA KUPITIA

**#1**

Rutgers - 16 Days Campaign - USA
https://16dayscwgl.rutgers.edu/
#16Days

**#2**

United Nations Women - 16 Days Campaign - USA
http://www.unwomen.org/en/what-we-do/ending-violence-against-women/take-action
#HearMeToo

**#3**

Prevent GBV Africa - 16 Days Campaign - UGANDA
http://preventgbvafrica.org/understanding-vaw/

# NAMBA ZA MSAADA WA KISHERIA

**Mashirika yafuatayo yanatoa bure msaada wa kisheria. Ukiwa na dharura piga bure namba 0800750035, 0700751010, 0800780100, 0800780070.**

Unaweza fika katika ofisi zetu kwa ajili ya ushauri na msaada wa kisheria kupitia anwani zifuatazo:
Women in Law and Development in Africa (WiLDAF) :
National Coordinator
Mikocheni A area, WiLDAF Street,
Block F, Plot No. 635
Po Box 76215, Dar es salaam,
Tanzania
+255 22 270 1995

Legal and Human Right Centre (LHRC)
Piga Bure Namba : 0800750035
www.humanrights.org

Tanzania Women Lawyers Association (TAWLA)
Piga Bure Namba : 0700751010
www.tawla.or.tz

Women and Legal Aid Centre (WLAC) :
Piga Bure Namba : 0800780100
www.wlac.or.tz.


Women in Law and Development in Africa (WiLDAF)
Piga Bure Namba : 0800780070
www.wildaftanzania.org

Tanzania Youth Alliance (TAYOA)
operates the National Health (Afya) AIDS Helpline
Piga Bure Namba 117
www.tayoa.org

# FUNGUKA!

## UKATILI DHIDI YA WANAWAKE NA WATOTO
## NI SUALA LA KITAIFA

## CHUKUA HATUA.



#HerSafetyMyResponsibility